# CHUKI HULA AKILI

**Na. MWANAWETU MMUNI**

**Hakimiliki©Mwanawetu Mmuni**
P. O Box 90,
Mtwara – Tanzania
Simu; +255 737966996
Baruapepe:
info@mwanawetubooks.co.tz

**© 2021**

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi.

## Nini maana ya neno chuki?

Chuki ni hali ya kutokuwepo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya, au hali ya kuwa na kinyongo. Wakati **Akili** ni uwezo wa mtu wa kujua kitu au jambo.

Chuki inaweza kujengwa na mtu binafsi kulinga na huruka ya mtu (hapendi kupata kwa mwenzie) au inaweza kutengenezwa na watu wasiopenda maendeleo (wapotoshaji).

Njia zote mbili zinaweza kumfanya mtu awachukie watu au mtu, au taasisi bila kuwa na uthibitisho wa kile anachokiamini

na kumsababishia kuwa na chuki.

Kuna watu hapa duniani hawajajua kama chuki inakula akili ya mtu.

Ukitaka kufanyakazi bila weledi hata kama una taaluma na ubunifu wa kutosha katika kufanya jambo hilo; beba chuki kwenye jambo lenyewe, au mtu aliyekutuma, au jamii unayoihudumia, au taasisi, au wafanyakazi wenzako.

a) **Chuki kwenye jambo lenyewe;**

Ukifanyakazi unayoichukia lazima upate matokeo mabaya au ya udanganyifu. Pia kwa upande wako binafsi lazima utajiumiza na kama uamini, kwa wale wanaotumia nguvu kutekeleza majukumu yao; lazima wapate na majeraha kwa kubondwa na vitu vizito, kumezwa na mashine, kuharibu mashine, kujigonga, kujikata kwa kutumia vifaa wanavyotendea kazi kama vile jembe kwa wakulima, kunaswa na vitu au nishati kama umeme au mashine.

Lakini hata wale wanaotumia maarifa kutenda kazi; yawapasa kuondoa chuki sababu matokeo yanaweza kuwa mabaya. Matunda ya chuki ni pamoja na usahaulifu, uongo ambao utauita utetezi, udanganyifu utakaoleta uchochezi, umaskini, uvivu kama vile mtu kuacha kujituma na kusubiri atumwe au asukumwe ili aendeleze chuki yake. Kupindishwa kwa taarifa (upotoshwaji) ili kukidhi mwendelezo wa chuki.

### b) Chuki kwa Mtu aliyekutuma kazi (Bosi/Mwajiri/tajiri)

Hali hii inajitokeza sana kwenye mashirika ya umma, taasisi binafsi, taasisi za serikali, makampuni na kwenye idara za ofisi mbalimbali ziwe binafsi au za umma.

Kuna watu wanajenga chuki katika kutenda kazi kwakuwa mtu aliyempa kazi au aliyemtuma hampendi hivyo kuichukia na kazi aliyopewa. Endapo kazi hiyo hiyo angelipewa na mtu mwingine hata kama angeambiwa aifanye

bure bila hata ya malipo au kwa mkopo; angelifanya kiukamilifu na kwa wakati.

Matokeo ya chuki hii inapelekea maendeleo kushuka hadi kwenye ngazi ya taifa.

Malalamiko ya wananchi kuhusu changamoto hadi zile za wilayani ambazo zingelisimamiwa vizuri na watendaji wa ngazi ya kijiji, kata, tarafa, halmashauri au wilaya maendeleo yangepatikana. Kutokana na chuki watakazofanyiana watendaji wa ngazi hizo, kunakuwa na uwezekano wa malalamiko au changamoto

kufika hadi ngazi ya Serikali Kuu au kumfikia Rais wa nchi na mwishowe kubebeshwa lawama na matusi kwa uzembe uliosababishwa na chuki za watendaji wa ngazi hizo za chini.

Hali hii haipo kwenye ngazi kubwa za serikali na mashirika pekee ambazo zinahitaji uteuzi na kuchaguliwa bali hata kwenye ngazi za utumishi wa umma na ngazi za familia.

*i) Ngazi ya familia*

Familia nyingi zinaendelea kuwa maskini kwa sababu ya chuki binafsi za wanafamilia.

Matokeo yake ni ongezeko la vifo visivyo na historia ya wazi, uchawi na fitina.

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya ndugu kutolea ushahidi kuwa ndugu zao wasipewe nafasi za uongozi au ajira. Kwa visingizio kuwa hawana uwezo, ilimradi wasiweze kunufaika na nafasi hiyo wakidhani watakuja kuwaringia hapo baadae kutokana na mafanikio (kuwazidi kiuwezo).

Wapo wanaofikiri chuki za familia zipo kwa ndugu wa kambo (wasiozaliwa nao) na

kuwaamini marafiki na ndugu wa damu.

Chuki ya mtu binafsi haichagui mtu wa Karibu wala wa mbali, wala kujitoa kwa mtu. Waweza mtu kujitoa kwa mwenzake kisha kulipwa kwa chuki na hasira.

*ii) Watumishi*

Chuki kwa watumishi sehemu za kazi ni kubwa ingawa inaendeshwa kwa kificho.

Inajidhihirisha kupitia upendeleo! Kama kuna watumishi wanapendelewa, kinyume chake kuna watu wanachukiwa.

Kwa kawaida; wanaochukiwa wanaitwa wavivu, wachochezi, wasio na weledi, wenye kiburi na matatizo mengine ya kibinadamu.

Inawezekana matatizo hayo yakawepo pia. Lakini kuna swali la kujiuliza; Kwanini changamoto za taasisi zinaendelea kuwepo wakati wenye hila tayari wameshatengwa? Kama kweli wale wachache wanaopewa kipaumbele kuwa ni watendaji wenye nidhamu na wachapakazi, kwanini bado kuna kazi zinaendelea kulala?

Chuki sehemu za kazi ni sumu kwa matokeo chanya ya taasisi na kusababisha kutoa huduma hafifu au bidhaa duni au zenye sumu endapo chuki hizo zitaendelezwa kwenye makampuni.

Wenye chuki wanadhani wanamkomoa Bosi, mwajiri au serikali. Kumbe wanarudisha nyuma maendeleo ya nchi, taasisi au jamii kwa kutoa huduma isiyoridhisha.

### *iii) Marafiki*

Rafiki ni mwanamke au mwanaume anayeaminiana na

mwingine na anayeshirikiana naye katika mambo mengi.

Watu wengi wanathubutu kutoa siri zao hata zile za aibu kwa watu wengine wanaowaamini (marafiki).

Wanaweza kuwa ndugu wa damu, au watu wenye rika inayolingana, au jinsi moja au jinsi tofauti. Lakini kwa mara chache kunakuwa na marafiki wenye umri unaotofautiana sana na Waswahili walishawapa majina marafiki hao na kuwaita “Somo” “mtani”.

Ubinafsi wa watu hawa wa karibu unaweza kupelekea

kuzaa chuki inayojificha na mwishowe kuleta madhara makubwa. Kwa kuwa matokeo yake yanakuwa ni ya ghafla. *Mfano kwa marafiki wa kike* wanaweza kuoneshana upendo na baadae kuvunjwa na mapenzi. Yaani mmoja akachukia baada ya mwenzake kupata mpenzi.

### c) Mapenzi

Mapenzi ni mwanzo wa chuki. Kila unachokipenda utataka kisiharibiwe au kupata madhara.

Gharama ya kulinda upendo inachangia kuumbwa kwa chuki na kuchafuana.

**Chuki inasababishwa na mambo yafuatayo;**

**Ubinafsi**; Mwanzo wa chuki ni mtu binafsi kuwa na mawazo ya; “*bora tukose sote au bora nipate mimi!”*

**Tamaa**, watu wengi wenye tamaa ya kuwa na kipato kikubwa bila kutia juhudi ya kutafuta mali hizo wanajikuta wakiwachukia wenye utajiri.

Ikitokea kiongozi kaongea jambo linaloonesha kuwazodoa matajiri au kusema jambo linaloonesha kuwashusha, wenye tamaa

wataonesha chuki zao waziwazi na utasikia wakisema; *“afadhali washushwe tulingane!”*

**Sababu za kiuchumi**; nazo zinachangiwa na kukithiri kwa unyonyaji. Upendo waleta huruma, hivyo watu wanashindwa kudumisha upendo wasije wakafirisika.

**Kisiasa**; hapa watu wanakuwa na chuki sisizo na msingi zinazosababishwa na wapambe.

Kuna watu wanakuwa vigeugeu kutokana na kuwa na chuki za watu kwa maslahi yao na wao kufuata mkumbo.

Matokeo yake ni kuwa na utajiri wa hewani usiokuwa na msingi kama vumbi angani. Kwa mfano, kupewa nafasi ya uongozi wenye sifa zitakazokupwaya na kupelekea kuangukia pua kisha kujikuta umejiharibia na kurudi nyuma sana kisiasa. Lakini wengine kujikuta wakiingia matatani baada ya kuonesha chuki kwa watu wasiolingana nao kiuwezo. Kwa mfano viongozi kwa viongozi wanaulinzi kutegemeana na uwezo wao lakini kibaraka ni rahisi kukamatwa na kuchukuliwa hatua endapo utabainika umevunja sheria.

Kwa upande wao watakuwa na wanasheria, madaktari na fedha nyingi za kuwawezesha kupata wakitakacho ili kuficha aibu (kujisafisha) endapo itatokea. Lakini kwa wapambe itashindikana.

**Kiitikiadi**. Itikadi na chuki ni vitu viwiwli tofauti. Kupishana kiitikadi kunadhiirishwa kwa hoja na sio chuki.

Mpishane na mpinzani wako kwa hoja na akikushinda ni vema ukikubali kushindwa na mpongeze mwenzako kisha jipange kupambania nafasi yako

ya kiitikadi bila chuki wala hasira.

Matokeo ya chuki za kiitikadi ni machafuko ya kisiasa, kurudisha nyuma maendeleo ya nchi, umaskini, na ufisadi.

**Imani**. Imani ya dini au misimamo mikali; kuwa na imani thabiti ya dini, isiwe ni chuki kwa watu wengine wenye imani tofauti.

Kutetea imani yako ni kuzingatia maagizo ya dini yako na ikitokea unamshawishi mtu kufuata imani yake, iwe ya kirafiki (kutongoza) badala ya kulazimisha na kuwajengea watu chuki.

Pia kwenye misimamo yeyote mikali hata ile ya kitamaduni kwa maana ya mila na desturi inahitaji kuvumiliana. Kwa mfano mila ya kukeketa watoto wa kike na wanawake. Miongo michache iliyopita ilionekana ni mila bora ya jamii husika. Lakini kila siku ziliposonga mbele iligundulika madhara ya kutekeleza mila hiyo (kukeketa) ni makubwa kuliko faida. Ndipo serikali na vyombo vingine vinavyotetea haki za binadamu vilipovalia njuga kukomesha mila hilo na kuiita potofu.

Sasa basi, yeyote atakayeendeleza mila hiyo

atakuwa ni mwenye misimamo mikali.

Ndiyo sababu watetea haki wanausia uvumilivu. Ukikosekana, kutapelekea chuki na matokeo yake ni kama ifuatavyo;

*Matokeo ya chuki ya kiimani;*

- Utengano
- Migogoro
- Machafuko ya kisiasa
- Vita
- Ugaidi
- Watoto wa mitaani
- Matumizi ya madawa ya kulevya
- Watoto yatima na wajane

- Umaskini uliokithiri
- Ufisadi
- Rushwa
- Siasa chafu zenye makundi
- Huduma duni za kijamii
- Kuenea kwa bidhaa zilizotengenezwa chini ya kiwango

***